OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASH AURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE-NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE
SLP 479,
NJOMBE.
24/05/2018 .

KUMB NA:Mtkss/Kdtv/Jon/VOL.03/2018

JINA LA MWANAFUNZI.....
S.L.P .....
WILAYA/MKOA.....

YAH.MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE, WILAYA YA WANGING'OMBE- MKOA WA NJOMBE.

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (form V) mchepuo wa..... Katika shule ya sekondari Mount Kipengere.Shule hii ipo wilaya ya Wanging'ombe katika kijiji cha Kipengere umbali wa kilomita(km) 52 Magharibi ya mkoa wa Njombe.Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi,stendi kuu Njombe,panda mabasi yaendayo Kipengere au Ikonda- Makete ,nauli ni Tsh 4000/= hadi Kipengere. Kufika shuleni waweza kutembea au kuchukua pikipiki kwa sh.2000/=(maarufu bodaboda).Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 10/ 07/ 2018 na Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 20/07/2018.

2.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

2.1**SARE ZA SHULE**

A.WAVULANA

- Mashati meupe mawili(2) ya mikono mirefu
- Suruali mbili,(rangi ya brown ya kuiva1 na rangi ya bluu bahari 1)
- Tai (rangi ya bluu bahari 1 na rangi ya brown ya kuiva)
- Sweta moja (linapatikana karibu na mazingira ya shuleni)
- Soksi nyeusi jozi mbili
- **Nguo za kazi:**suruali nyeusi 1 pamoja na t-shirt (t-shirt inapatikana shuleni kwa tsh:10,000/=)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu na vyenye soli fupi.
- **Vifaa vya michezo** : track suit nyeusi yenye mkanda mweupe pamoja na raba za michezo za ngozi jozi moja.
- Jacket jeusi moja na lisiwe 'over size',rangi mchanganyiko michoro na maandishi yoyote .

B.WASICHANA

- Sketi mbili zinazofika kwenye magoti (rangi ya brown ya kuiva 1 na rangi ya bluu bahari 1) mshono umeambatanishwa kwenye fomu .
- Suruali mbili,(rangi ya brown ya kuiva 1 na rangi ya bluu bahari 1)
- Tai (rangi ya bluu bahari 1 na rangi ya brown ya kuiva 1)
- Sweta moja (linapatikana karibu na mazingira ya shule)
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Nguo za kazi(shamba dress) gauni 1 lenye rangi ya damu ya mzee na t-shirt (t-shirt inapatikana shuleni tsh: 10,000/=)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi pia vyenye kufunika miguu
- **Vifaa vya michezo** : track suit nyeusi yenye mkanda mweupe pamoja na raba za michezo za ngozi jozi moja.
- Jacket jeusi moja na lisiwe 'over size',rangi mchanganyiko michoro na maandishi yoyote .
- Wanafunzi wa kiisilaamu hijabu nyeupe ni kwa ajiri ya darasani na hijabu ya rangi ya pink ,na mtandio wake itavaliwa nje ya muda wa darasani.

2.2 **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

(a)Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/=.unatakiwa kulipa Tsh 35,000/= kwa muhula na zilipwe kutumia akaunti ya shule .Na **60601000017** katika benki ya NMB (tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye hati ya malipo ya bank na iwasilishwe anaporipoti shule)

(b) Michango mingine ni:-

i. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa thamani
ii. shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitaambulisho shule
iii. shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. shilingi 15,000/= kwa ajili ya wapishi,
v. shilingi 5000/= walinzi
vi. shilingi 5,000/= tahadhari
vii. shilingi 10,000/= gharama ya umeme na matengenezo

JUMLA ya ada na michango mingine kwa mwaka ni tsh: 150,000/= fedha yote ilipwe kupitia akaunti ya shule 60601000017 bank ya NMB

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream bunda 1 (kwa mwaka) karatasi za A4
ii. vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa kwenye fomu)
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
iv. Mashuka (rangi ya bluu bahari 1 na rangi ya pinki 1)
v. ,Blanketi zito moja ,mito,foronya (rangi ya bluu bahari 1 na rangi ya pinki 1)
vi. Scientific calculator kwa wanaosoma sayansi

vii. Godoro la futi $2_{1/2}$ x 6
viii. Vyombo vya CHAKULA
ix. Ndoo mbili ndogo
x. Ndala
xi. Sanduku la chuma (tranker)
xii. Vifaa vya usafi kulingana na tahasusi

a. **HGK** panga-1 ,slesha-1 ,mifagio ya ndani (hard broom 1,soft broom 1na rubber squeezer
b. CBG Slesha 1 ,jembe-1 **,** mifagio ya ndani (hard broom 1,soft broom 1na rubber squeezer
c. HGE Slesha-1 reki-1 , mifagio ya ndani (hard broom 1,soft broom 1na rubber squeezer
d. PCB Slesha-1, jembe-1, mifagio ya ndani (hard broom 1,soft broom 1na rubber squeezer

NB HAKIKISHA JEMBE LINAKUWA NA MPINI

xiii. Madaftari makubwa(counter books quire 4) kiasi cha kutosha yasiyopungua 15 na daftari ndogo 10 quire 2 mitihani ya mwezi.

2.5: **MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA**

(a)Cheti cha kuzaliwa.

(b)Kila mwanafunzi atajigharamia kwa matibabu wakati wote awapo shuleni.

(c)Fedha ya matumizi itahifadhiwa kwa mkuu wa shule.

(d)Mwanafunzi haruhusiwi kuja na **SIMU YA MKONONI** kwa sababu yeyote ile hivyo kutapelekea mwanao kufukuzwa shule pindi atakapogundulika kumiliki simu .

Hivyo basi mwanao anashauriwa kuwa na namba zifuatazo kwa mawasiliano ili aweze kufika shule (kwa mawasiliano atembee na namba zifuatazo:- **0768661887 /0718831747** mkuu wa shule / 0758126961makamu mkuu wa shule).

e) Mwana ajapo shule anatakiwa kuvaa track suti ya shule ambayo ni nyeusi yenye michirizi myeupe

f).Mwanao haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani za aina yeyote ile licha ya zile zilizo ainishwa kwenye fomu hii na ikiwezekana kwa dhana hii mnunulie jozi mbili za nguo za nje na michezo .

3.0: **SHERIA ZA SHULE**

3.1Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu N a.25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara tu anapowasili shuleni;

(a)Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
(b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli(shughuli za kitaaluma na shughuli za nje).
(c)Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(Evening Preparation).
(d)Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shule wa kati wote wa uanafunzi wako.
(f)Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

(g)Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa shuleni(nguo zingine nje ya sare / maagizo ya shule haziruhusiwi).

(h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(i)Lugha chafu, matusi,ugomvi,fitina,kupiga/kupigana ni mwiko kabisa.

(j)Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ni mwiko kwa wanafunzi.

(k)Wizi wa aina yoyote ni mwiko kwa mwanafunzi.

(l)Uharibifu na upotevu wa mali binafsi na mali ya umma ni kosa kubwa.

(m)Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa akiwa bado mwanafunzi.Akibainika atafukuzwa shule mara moja,aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na mahusiano/uhusiano wa kimapenzi.Akibainika adhabu yake ni kufukuzwa shule.

(n)Wageni wataruhusiwa kuwaona/kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu,kila Jumapili ya kwanza ya mwezi.

(o)Ni mwiko kwa mwanafunzi yoyote kwenda nyumba za walimu na wafanyakazi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi.

(p)Ni marufuku kwa Mwafunzi kuwa na simu ya mkononi.

(q)Mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku na haramu.

(r)Mwanafunzi atafuata maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(s)Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufukuzwa shule.

3.2**Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi afukuzwe shule;**

i. Wizi
ii. Uasherati,ushoga ,ubakaji, kuoa au kuolewa
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine,kubeli n,k
iv. Uvutaji wa sigara
v. Kupiga au kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule na makosa mengine ya jinai
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu au walezi na jamii kwa ujumla
ix. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
x. Kukataa adhabu kwa makusudi
xi. kumiliki **SIMU YA MKONONI** shuleni au vifaa vyovyote vile vinanavyohusiana na simu kamavile betri na simu kadi n.k
xii. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina
xiii. Kunyanyapaa au uonevu wa aina yoyote
xiv. Kuweka mimba au kupata mimba
xv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kama kunywa sumu n.k

.....
MHANGA B.B
MKUU WA SHULE

FOMU NA 1 KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI

A: MWANAFUNZI

1. Jina kamili.....
2. Shule ya "O" Level uliyosoma.....
3. Namba ya mtihani.....
4. Tarehe ya kuzaliwa.....
5. Nakubali nafasi niliyopewa/siitaki apewe mwingine (kata lisilohusika)
6. Nakiri/naahidi kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
7. Sahihi.....

B:AFISA MTENDAJI

Jina.....

Kijiji/mtaa ..... Wilaya..... Mkoa.....

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ..... ni mkazi wa kijiji hiki/mtaa huu na ni raia wa Tanzania.

Sahihi..... Muhuri..... Tarehe.....

C: MZAZI/MLEZI

Jina.....

Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Kipengere sekondari,na kwamba atafuata sheria, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa shule na vinginevyo adhibiwe.Pia atalelewa katika dini ya .....

FOMU NA.2. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

JINA LA MWANAFUNZI.....

TAREHE YA KUZALIWA .....

JINSIA.....

UMRI.....

MAHALI UNAPOISHI..... WILAYA.....MKOA.....

SIMU NA. .....

JINA LA BABA..... YUPO HAI?.....

JINA LA MAMA..... YUPO HAI?.....

ANUANI.....

SIMU NA. .....

KAZI YA MZAZI/MLEZI.....

MIMI .....NAKIRI KWAMBA TAARIFA NILIZOTOA NI SAHIHI.

SAHIHI..... TAREHE.....

NB.TAARIFA ZA UONGO/ZISIZO SAHIHI ZITAPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

FOMU NA 3. MEDICAL EXAMINATIONS

(T o be completed by medical officer)

1. Pupil's name.....

2. Age.....

3. Blood count (white and red).....

4. Stool examination.....

5. Syphilis or/and other venereal diseases test.....

6. T.B test.....

7. Eye test.....

8. Ears.....

9. Abdomen.....

10. Spleen.....

11. Urine for plamo test.....

ADDITIONAL INFORMATION

If any e.g. physical defeats, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases etc.....

.....

I CERTIFY THAT HTE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

Station..... Signature.....

Date..... Designation.....

.....

FOMU NA 4. PLEASE IF POSSIBLE COME WITH THE FOLLOWING BOOKS/REFERENCE MATERIALS RELEVANT TO YOUR COMBINATION AS LISTED BELOW:-

1.history

i. Major in Africa history
ii. Major events in Africa history..... by MWIJAGE
iii. The political, economy and imperialism.....by
iv. Africa since 1800-4th edition.....by
v. The making of modern Africa.....by
vi. How Europe underdeveloped Africa .....by
vii. The 20th century.....by Duff M.N
viii. Europe from 1815.....by Peacock

2.geography

i. Certificate of geography (oxford).....by Mary M ugo,Robert Karrugat and Paul Kibuuka
ii. General geography in diagrams.....by R.B Bunnet
iii. Photography interpretation and elementary surveying for secondary level New Edition by S.E Dura
iv. Regional geography .....by Nyangwine and Msabila
v. Certificate human and economic Geography .....by Morgan and Leong Ghang

3. Chemistry

i. A. lvel chemistry (4th Edition) .....by E.N Ramsden
ii. Physical chemistry for A. level and 1st year undergraduate student – Mzumbe book project
iii. Inorganic chemistry (part A and B)..... Mzumbe book project
iv. Organic chemistry (part A and B)..... Mzumbe book project
v. Chemistry in Action ..... Michael Freemantle

4. Biology

i. Biological science..... by Tylor
ii. Biology..... by Silvia and Marder
iii. Biology (Guide to dissection).....by Rewelt and Murray
iv. Dissecting Kit (Kila mwanafunzi awe nayo)

5. General studies

Understanding advanced level general studies by J.Bigirwamungu & S.Deogratius

General Studies Notes(for A-level form v-vi).....by Mshiu and Nyangwine

6. KIWAHILI

Ushairi

i. kimbunga.....G.Gora (TUKI) 1994
ii. chungu Tamu .....T.A Mvungi
iii. Mapenzi bora ..... M.s Khatibu

Riwaya

i. Vuta N'kuvute .....Shafi A. Shafi
ii. Kufikirika .....S.Robert
iii. Mfadhili .....Hussein Tuwa
iv. Usiku utakapo kwisha ..... Mbunda Msokile

Tamthilia

i. Morani .....E.Mbogo
ii. Kivuli kinaishi ..... saida Mohamed
iii. Kwenye ukingo wa Thim ..... E.Hussein
iv. Nguzo mama ..... (DUP) 1982

7.PHYSICS

i. Physics book by S. Chand I& II
ii. Physics book by Tom Dancan
iii. Physics book by Roger Manchester
iv. Principle of physics by Nelkon
v. University physics book (U.P)
vi. Comprehensive physics
vii. Understanding physics
viii. Numerical physics

8.ECONOMICS

i. Modern economics by Mudida
ii. Economics simplified by Saleem
iii. Principles of economics by Ahuja
iv. Positive economics 8^{th} edition by lipsey
v. Introduction to economics theory by Gupta

MUUNDO WA VAZI LA MWANAFUNZI WA KIKE



NB: Sketi lazima ifike kwenye magoti.